

**Uzalishaji wa Tafsiri Sadifu katika Matini za Majukwaa ya Kidijiti:
Harakati na Changamoto**

Mark Odawo
Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Rongo

odawomark14@gmail.com

na

Carren Nyandiba
Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu cha Rongo

cnyandiba@rongovarsity.ac.ke

Ikisiri

Makala hii inaangazia harakati na changamoto katika kuzalisha tafsiri sadifu katika majukwaa ya kijiditi. Makala inaangazia matini zilizotafsiriwa kutoka lugha chanzi ya Kiingereza kwenda lugha lengwa ya Kiswahili. Uteuzi wa kimakusudi ulitumiwa kupata sampuli sadifu kutoka majukwaa ya tuko.com na bbc.com. Ukusanyaji wa data uliofanywa kwa takriban miezi mitatu: kuanzia Julai hadi Septemba mwaka wa 2018 ulihusu usomaji wa matini ili kudondoa data yakini kupitia rununu na tarakilishi. Matini zilipakuliwa kutoka mtandaoni na kunakiliwa kwenye daftari kabla ya kuchanganuliwa. Utafiti huu umebainisha kuwa wafasiri walijitahidi kuzalisha tafsiri sadifu zenye utoshelevu wa kimaana. Hata hivyo, kwa kiasi kikubwa, harakati hizo za kuzalisha tafsiri sadifu zimekumbwa na changamoto ambazo zimedhihirika kupitia ujitokezaji wa tofauti za kiutamaduni kati ya lugha chanzi na lugha lengwa, uchechefe wa visawe vya kisayansi na kiufundi, tafsiri tenge ya misamiati ibuka na ugumu wa kutafsiri misamiati ya TEHAMA. Makala hii inapendekeza kuwa, pana haja ya kuweka mikakati ya kuboresha tafsiri ya matini tepe zinazotafsiriwa katika majukwaa ya kidijiti ili kuhakikisha usadifu wa jumbe zinazowasilishwa kwa hadhira lengwa katika harakati za kufanikisha mawasiliano timilifu.

Dhana za Msingi: Tafsiri, sadifu, majukwaa ya kidijiti

Utangulizi

Shughuli za kila siku za binadamu humhitaji kutumia lugha kujieleza, kupashana taarifa na kupitisha maarifa. Kauli kuwa jamii za binadamu ulimwenguni ni za asili na tamaduni tofauti humaanisha kuwa haziwezi kuelewana kikamilifu na kupashana maarifa zinapotumia lugha zao za asili hupelekea haja ya kuhawilisha maana ya matini kutoka lugha moja hadi lugha nyingine ya wapokezi wa ujumbe kupitia taaluma ya tafsiri. Kama wanavyosema Wanjala (2011) na Mwansoko (2016), tafsiri kwa dhati yake ni daraja linalounganisha jamii mbalimbali zenye lugha zinazotofautiana na kwamba, bila tafsiri isingewezekana kwa jamii hizo kupata maarifa, ujuzi na utamaduni wa jamii nyingine. Mwansoko (*keshatajwa*) anashadidia kuwa lengo la uhawilishaji wa mawazo au ujumbe wa maandishi uliomo katika lugha chanzi (kuanzia hapa LC) kwenye lugha lengwa (kuanzia hapa LL) ni kufanikisha mawasiliano baina ya wazungumzaji wa lugha zinazotofautiana. Hivyo basi, mfasiri, anahitaji kuchakata tafsiri kwa usadifu ili kumfaidisha mpokeaji wa ujumbe. Kwa kuwa tafsiri imekuwa muhimu katika kutagusanisha jamii ya kimataifa na kufanikisha mawasiliano baina ya wazungumzaji wa lugha tofauti duniani, taaluma hii inatoa mchango mkubwa sana katika kuendeleza utandawazi (Matundura, 2007; House, 2016).

Wataalamu mbalimbali kama vile Catford (1965), Nida na Taber (1969), Larson (1984), Newmark (1988a), Mwansoko (1996), na Wanjala (2011) wanaafikiana kuwa tafsiri ni mchakato wa mawasiliano unaohusu uhamishaji wa maana na ujumbe ulio katika LC hadi LL. Lengo kuu la tafsiri ni kuwasilisha ujumbe uliomo kwenye matini chanzi (kuanzia hapa MC) kwa kutumia matini lengwa (kuanzia hapa ML) ili kuathiri hadhira lengwa (kuanzia hapa HL) kwa namna inayofanana na ile waipatayo

hadhira chanzi (kuanzia hapa HC). Kwa mantiki hii, tafsiri ina uhusiano unaoipa ML hadhi ya kuchukuliwa kama toleo jipya la MC.

Kuchipuka kwa mielekeo na mitazamo katika taaluma mbalimbali za kisayansi, kiufundi, kisheria, kibiashara na katika nyanja nyinginezo za kimaendeleo katika ngazi ya kimataifa, kumezidisha haja ya kutafsiri vitabu, magazeti, majarida na kazi nyinginezo ili kuwezesha usambazaji wa maarifa katika kufanikisha mawasiliano timilifu. Oduori (2008) anasema kuwa taaluma zinavyopanuka, uvumbuzi huendelea kuwepo. Maarifa yanayotokana na uvumbuzi huo huhitaji kusambazwa ili kuwafikia watu katika upande mwingine wa ulimwengu kwa lugha wanayoielewa vizuri. Hivi ni kusema kuwa tafsiri inategemewa sana katika kufanikisha mawasiliano na kusambaza maarifa katika dunia ya leo inayoendelea kuwa kijiji kidogo.

Maendeleo katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yamechangia mabadiliko makubwa katika uwasilishaji wa habari. Hii ina maana kuwa pana mwelekeo wa kuhama utegemezi wa nyenzo zilizozoeleka za kusambaza taarifa kama vile redio, televisheni, magazeti na majarida. Matundura (2007) anasema kuwa nyenzo hizi, wakati mwingine, hupasha habari tafsiriwa zilizo na mapungufu. Kama anavyosema Shitemi (2007), mawasiliano ya kiTEHAMA hasa katika sanaa za burudani, maonyesho ya filamu na uhabarishaji katika vyombo vya habari yamepanua dhima ya tafsiri za kielektroni. Leo, utandawazishaji wa taarifa umewezeshwa kwa wepesi wa ajabu kupitia majukwaa ya kidijiti (kuanzia hapa MK). Japo uwasilishaji wa taarifa zilizotafsiriwa mtandaoni kwa Kiswahili ni tukio la miaka ya hivi majuzi, watu wanaofuatilia na kutegemea MK ili kupata habari huzidi kuongezeka kila uchao.

Kwa mujibu wa Tam na wenzake (2007), MK ni nyenzo ya kuzalisha na kuwasilisha maarifa ambayo yanaendelea kutumiwa kwa wingi katika kizazi cha sasa kutokana na uwezo wake wa kutandawazisha taarifa na matukio yanayochipuka kwa wepesi wa ajabu. Safko na Brake (2009) wanafafanua MK kama vyombo vya mtagusano ambavyo kwavyo pana harakati za watu kukusanya na kusambaza taarifa, maarifa, na maoni kuhusu masuala anuwai. Wanasema kuwa midia hii inahusisha matumizi ya kimtandao katika uzalishaji na usambazaji wa matini andishi, matini sikizi, matini za picha na video. Kijelezi cha Waters na Lester (2010) nacho kinafasiri MK kama midia inayotumiwa na umma kuwasiliana, kutumiana jumbe, kutagusana katika makundi, kutoa maoni kuhusu masuala yanayojadiliwa na kuhakiki matini mbalimbali zinazosambazwa.

Watu wengi wanachangamkia majukwaa haya kutokana na uwezekano wa kupata taarifa nyingi mahali popote punde tu zinapochipuka. Taarifa ambazo, kimsingi, huandikwa kwa LC ya Kiingereza pia huifikia umma kutokana na tafsiri katika LL yoyote kupitia MK. Hata hivyo, changamoto za kutafsiri taarifa zinazozalishwa katika MK zimekuwa kikwazo dhidi ya dhima ya kimsingi ya lugha ya kufanikisha mawasiliano na kusambaza maarifa. Ni kwa misingi hii ambapo makala hii inaangazia ukakasi katika kutafsiri matini kwenye majukwaa ya kidijiti.

Methodolojia

Makala hii ni zao la utafiti uliofanywa katika MK. Katika utafiti huu, uteuzi wa kimakusudi ulitumiwa ili kupata sampuli sadifu kutoka majukwaa ya *tuko.com* na *bbc.com*. Majukwaa haya yaliteuliwa kwa sababu huwa na matini nyingi zaidi zilizotafsiriwa moja kwa moja kutoka Kiingereza hadi Kiswahili kwa uwazi zaidi ikilinganishwa na majukwaa mengine kama vile

Facebook, Twitter, na WhatsApp. Ukusanyaji wa data ulihusu usomaji wa matini ili kudondoa data yakini kutoka MK kupitia rununu na tarakilishi. Matini zilizotambuliwa na kudondolewa ni zile zilizoangazia ufumaji wa maana katika matini za kisiasa, kijamii, kiuchumi na michezo zilizotafsiriwa kutoka LC ya Kiingereza kwenda LL ya Kiswahili. Ukusanyaji wa data ulifanywa kwa takribani muda wa miezi mitatu: kuanzia mwezi Julai hadi Septemba mwaka wa 2018. Matini zenye data zilizohitajika zilipakuliwa kutoka mtandaoni na kunakiliwa kwenye daftari kabla ya kudondolewa, kupangwa na kuchanganuliwa. Data zilizokusanywa zilizumuisha misamiati, istilahi, virai, vishazi, na sentensi. Kimahsus, tulijikita katika kuchanganua data husika kwa kulinganisha na kulinganua MC na ML. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kwamba harakati na changamoto katika kuzalisha tafsiri sadifu zimedhihirika kupitia masuala mbalimbali ambayo yamefafanuliwa katika makala hii.

Matokeo ya Utafiti

Katika kuhawilisha ujumbe, mfasiri anatarajiwa kuzalisha ML inayonasibishwa na MC. Jaribio la kuibua athari sawia ya kisemantiki kwa HL humhitaji mfasiri kuwa mwangalifu ili kuchunguza vivuli vyote vya maana vinavyodhihirika katika matini. Hata hivyo, haiwi rahisi kufikia upeo huu kwa sababu katika jaribio la kuhawilisha maana ya kimatini, mfasiri, wakati mwingine, hukumbana na matatizo yanayosababisha upungufu wa muumano wa maana.

Kwa mujibu wa Newmark (1991), na Kihore (2005), ni nadra kupata tafsiri kamilifu isiyo na dosari. Mwansoko na wenzake (2006) nao wanaeleza kuwa kiini cha upungufu katika tafsiri ni mvutano unaotokana na tofauti za

kiutamaduni, kihistoria, kiisimu, kimaumbo, kimiundo, na kimazingira kati ya LC na LL.

Japo kuna matatizo yanayojikita katika umilisi mfinyu wa lugha zote mbili zinazohusika katika kadhia ya tafsiri, changamoto nyingine zinafungamana na aina ya matini inayotafsiriwa na miundo ya lugha zinazohusika miongoni mwa nyingine. Utafiti huu umebainisha kuwa harakati za kuzalisha tafsiri sadifu ya matini katika MK zimelemazwa na ujitokezaji wa tofauti za kiutamaduni kati ya LC na LL, uchechefe wa visawe vya kisayansi na kiufundi, tafsiri tenge ya misamiati ibuka, na ugumu wa kutafsiri misamiati ya TEHAMA.

Tofauti za kiutamaduni kati ya LC na LL

Kwa mujibu wa Newmark (1988b), utamaduni ni mkusanyiko wa mila na desturi za jamii inayotumia lugha moja mahsusi kama njia yake ya mawasiliano. Musyoka (2019) anasema kuwa, kwa sababu lugha hupata maana katika utamaduni wa wazawa wa lugha husika, lugha na utamaduni huelekea kuwa pande mbili za sarafu moja. Kwa upande wake, Elyildirim (2008) anasema kuwa lugha haieleweki nje ya muktadha wa utamaduni wake na kwamba utamaduni huhifadhiwa na kusambazwa kupitia lugha. Nida (1964) anaeleza kwamba mfasiri anapochakata tafsiri, huwa anatangamanisha tamaduni mbili tofauti. Kwa mantiki hii, tafsiri fanifu hufikiwa pale ambapo mfasiri anaelewa tofauti na mapatano ya kiutamaduni yanayoshehenezwa katika lugha zote mbili. Mbali na kueleza jinsi jamii fulani mahsusi zinavyoishi, utamaduni hupambanua mazingira ya jamii hiyo. Mazingira hayo hutazamwa kama ghala la kuchotea malighafi zinazofuma lugha ya jamii hizo.

Kwa sababu ya uwepo wa vitu na hali tofauti katika mazingira, watu hujitokeza na dhana mbalimbali za kutajia vitu na hali zinazopatikana katika mazingira yao. Kwa sababu hii, inakuwa vigumu kupata maneno sawia ya kurejelea dhana zinazopatikana katika tamaduni na mazingira tofauti. Kinachomaanishwa hapa ni kwamba kila lugha hutumia muonoulimwengu tofauti katika kueleza uhalisia unaoendesha jamii inamotumika. Shiyab (2006) anadai kuwa si rahisi kupata ML iliyo na mshabaha kamili na MC, hasa kutokana na matumizi ya lugha mbili zenye tamaduni tofauti. Japo maoni haya hayapaswi kutumiwa kama kisingizio cha tafsiri dufu, yanatuonesha uhalisia wa dosari zinazoweza kutokea katika kadhia ya tafsiri. Kwa upande wake, Jilala (2016) anashadidia kuwa, wakati mwingine, dhana zinazofungamana na utamaduni mahsusi wa jamii inayozungumza LC zinapotafsiriwa katika LL yenye utamaduni tofauti na ule wa LC, hukengeushwa kutokana na msigano wa tamaduni hizo. Anaendelea kudai kuwa, ili kufikia ushikamani wa maana na ujumbe baina ya MC na ML, mfasiri wa matini ya kiutamaduni anatakiwa kuelewa na kuzingatia visawe vya kiutamaduni vya LC katika LL au kuteua mbinu itakayomwongoza katika kueleza utamaduni chanzi kwa kutumia lugha ya utamaduni lengwa.

Mara nyingi, inabainika kwamba neno fulani katika MC linarejelea dhana ambayo haifahamiki wala kueleweka katika LL kwa njia ya kutumia neno moja. Hali hii huhitaji maelezo ili kubainisha maana. Neno linalorejelewa hapa huenda lihusiane na dhana ya imani fulani, taratibu za jamii, mchakato wa maandalizi ya chakula cha aina fulani, desturi, na miiko. Nida (1964) anasema kuwa utamaduni huwa changamani zaidi ya lugha kwa sababu, huku lugha ikiwakilisha utamaduni kupitia ishara tamkwa, utamaduni

hufuma imani za jamii ambazo lugha haiwezi kupambanua kwa ukamilifu. Kwa sababu, hii inakuwa vigumu kuakisi masuala yote ya kiutamaduni katika tafsiri. Mifano ifuatayo inadhihirisha ugumu wa kutafsiri maneno yanayorejelea dhana zisizozoeleka katika utamaduni wa LL.

Jedwali Na. 1: Tafsiri Kengeushi ya Matini za Tamaduni Baidifu

Matini Chanzi	Matini Lengwa	Chanzo
<i>The dinner</i> was attended by top travel operators and investors seeking partnerships to accelerate America investments in Kenya as the direct flights were expected to open new frontiers in enhancing tourism, trade and investment opportunities.	<i>Maakuli</i> hayo yalihudhuriwa na vigogo wa usafiri na wawekezaji wanaotaka kuhakikisha uwekezaji wa Amerika na Kenya huku safari za moja kwa moja zikitarajiwa kufungua mikondo mipya katika kuboresha nafasi za utalii, biashara na uwekezaji.	<i>tuko.com</i>
UEFA set to investigate Juventus over Cristiano Ronaldo’s mega signing this summer. The European football governing body is planning to investigate the deal for <i>financial fair play discrepancy</i> . Ronaldo ended his nine year reign with current European champions Real Madrid after the World Cup...The 33 year old joined the Old Lady in a mega deal valued around Ksh 13.9 billion from Real Madrid after spending nine seasons at the Santiago Bernabeu. His arrival at the Allianz Arena meant Juve spent a total of Ksh 28.6 billion (£217 million) during the transfer window which saw the likes of Douglas Costa na	UEFA kuchunguza Juventus kuhusiana na <i>malipo ya juu</i> kumpata Cristiano Ronaldo. Shirika la Kandanda Uropa (UEFA) laazimia kuchunguza mkataba wa kifedha unaohusisha Juventus. Ronaldo alimaliza kandarasi yake ya miaka tisa na Real Madrid baada ya Kombe la Dunia... Mchezaji huyo aliye na miaka 33 alijiunga na Juventus baada ya kutia sahihi mkataba wa thamani ya Ksh 13.9 bilioni kuondoka Real Madrid baada ya kukaa miaka	<i>bbc.com</i>

<p>Joao Cancelo join the Turin club. However, Calcio Mercato claims the deal could come back to haunt them as they are set to be scrutinized by the governing body to check their spending in the last window. Juventus however may argue they balanced their financial books after selling Mattia Caldara and Gonzalo Higuain.</p>	<p>tisa Santiago Bernabeu. Kuwasili kwake Allianz Arena ilimaanisha kuwa Juventus ilitumia Ksh 28.6 bilioni wakati wa uhamisho huo ambapo wachezaji wengine kama Douglas Costa na Joao Cancelo walijiunga na Turin club. Hata hivyo, Calcio Mercato alidai kuwa huenda mkataba huo ukawasumbua baadaye kwani wanalengwa kuchunguzwa na UEFA kuhusiana na ilivyotumia pesa. Lakini huenda Juventus ikajitetea kwa kusema kuwa iliuzia Mattia Caldara na Gonzalo Higuain kabla ya kumpa kandarasi Ronaldo.</p>	
<p>A less powerful quake earlier on Friday had killed at least one person and injured at least 10 in the smaller fishing town of Donggala. In Palu, hundreds of people had been preparing for a <i>beach festival</i> that was due to start on Friday night...The main airport in Palu has been losed since the tsunami hit.</p>	<p>Tetemeko hili lilianza kwa kutangulia kwa tetemeko lingine dogo liliua mtu mmoja na wengine 10 kujeruhiwa wakiwa katika soko dogo la samaki huko Donggala. Mjini Palu, Mamia ya watu walikuwa wanajiandaa kwa ajili ya <i>tamasha</i> lililokuwa linatarajiwa kuanza ijumaa jioni.</p>	<p><i>bbc.com</i></p>

Kwa mujibu wa Jedwali Na. 1, neno *dinner* limetafsiriwa kama *maakuli* katika matini ya kiuchumi. TUKI (2006) inaeleza *dinner* kama mlo mkuu wa siku. Kwa mujibu wa TUKI (2013), *maakuli* ni anuwai ya vyakula au chakula tu. Kwa maana hii, *maakuli* huwakilisha chakula kwa jumla ambacho kinaweza kuliwa wakati wowote ule. *Dinner* ni mlo mkuu wa siku na, aghalabu, huliwa kuanzia saa 6 mchana na kuendelea. Upotofu wa maana unaotokana na tafsiri hii umeathiriwa na utamaduni baidifu wa LC na LL. Lugha mbili au zaidi zinaweza kubeba tamaduni zinazohusiana pale zinapotokana na lugha mame moja na zinapokuwa na historia ndefu ya mtagusano. Msamiati wa lugha, kwa kiwango kikubwa, hujenga maana ya maneno kutokana na utamaduni na jamii inayozungumza lugha hiyo.

Kwa mujibu wa Nida (1964), vipengele vya kiutamaduni huainishwa katika ekolojia, violwa, mila na desturi, siasa, na dini. Tofauti za mila, desturi na imani huweza kuakisiwa katika tabia za ulaji, unywaji, uvaaji nguo, mapenzi, ndoa, na ada nyingine za kijamii. Kimsingi, katika utamaduni wa Kiswahili, chakula huliwa mara tatu kwa siku, yaani kiamsha kinywa, chamcha na chajio. Kwa upande mwingine, Waingereza wana *Breakfast, Lunch, High tea, Dinner, Supper* na *Cock tail*. Kwa mujibu wa haya, *maakuli* ni neno la jumla ambalo halibainishi kwa utondoti neno *dinner* ambalo linadokeza aina ya chakula na wakati wa kukila. Mwansoko (2016) anasema kuwa tafsiri hizi za kijumla hupoteza vionjo vya kisanii vinavyopatikana katika MC na kupunguza uzito wa maudhui na thamani ya ujumbe wa MC katika ML.

Katika matini ya michezo kutoka jukwaa la *bbc.com* ambapo Shirikisho la Kandanda la Uropa (UEFA) linachunguza klabu ya Juventus kuhusiana na ilivyotumia fedha katika usajili wa wachezaji, data *financial fair play*

discrepancy imetafsiriwa kumaanisha *malipo ya juu*. Dhana inayotolewa katika MC ni kuwa, kwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 28.6 katika usajili wa wachezaji watatu, yaani Cristiano Ronaldo, Douglas Costa, na Joao Cancelo, klabu ya Juventus ilipiku kiwango kinachoruhusiwa na Shirikisho la Kandanda la Uropa ikilinganishwa na klabu nyinginezo.

Sheria ya mchezo wa kandanda hairuhusu klabu yoyote kutumia uwezo wake wa kifedha kusajili wachezaji wengi na wenye gharama ya juu kwa sababu kufanya hivi ni kujiinua na kujiweka katika hali nzuri ya kushinda mataji mengi ikilinganishwa na klabu nyingine zisizo na ukwasi wa kiwango hicho cha kifedha. Dhana hii ndiyo inayowakilishwa na *finacial fair play discrepancy*. Kufuatia maelezo haya, kutafsiri istilahi hii ya michezo kama *malipo ya juu* kunatoa maana ya kijumla na, hivyo, kushindwa kuibua ujumbe uliokusudiwa. Imekuwa vigumu kwa mfasiri kutafsiri istilahi hii kwa sababu LL haina ufungamano mkubwa na mchezo wa kandanda ambao una chimbuko lake katika nchi za Ulaya. Waaidha, mchezo wa kandanda haujafikia kiwango cha vilabu kutumia pesa nyingi kusajili wachezaji katika sehemu za utamaduni wa Kiswahili.

Aidha, katika matini hii, *beach festival* imepewa tafsiri ya *tamasha*. MC ilidhamiria kuweka wazi aina ya tamasha ambayo wenyeji wa Indonesia walikuwa wakijitayarisha kwayo. Kadhalika, kuwepo kwa neno *beach* katika *beach festival* kunadokeza pia mahala ambapo matamasha hayo yangefanyika, yaani ufukweni. *Tamasha* ni neno la jumla lisiloweka wazi aina ya tamasha na mahali pa kufanyia tamasha lenyewe. Inawezekana kuwa mfasiri alishindwa kuzua istilahi ya kurejelea dhana hii katika LL, na, hivyo, kuishia kutumia neno la jumla. Hii ni kwa sababu aina ya sherehe inayorejelewa katika MC inafanyika nchini Indonesia na haina uhusiano na

utamaduni wa LL. Kulingana na maoni yetu, matumizi ya istilahi *tamasha la wazi* yangeafiki zaidi maana iliyodhamiriwa.

Uchechefu wa visawe vya kisayansi na kiufundi

Changamoto nyingine ya kupata tafsiri sadifu imesababishwa pia na uchechefu wa visawe halisi vya kurejelea baadhi ya zana za kisayansi na kiufundi. Hali hii imepelekea matumizi ya istilahi za kijumla kuhawilisha dhana hizi, na, hivyo, kuzalisha tafsiri dufu. Matini za kiufundi katika Jedwali Na. 2 lifuatalo zinabainisha ukengeushi huu wa kiufasiri.

Jedwali Na. 2: Tafsiri Kengeushi ya Matini za Kisayansi na Kiufundi

Matini Chanzi	Matini Lengwa	Chanzo
A total of 11 Kenya Power managers face over four economic crimes according to Director of Public Prosecutions. The 11 and directors of Muwa Trading company allegedly conspired to purchase <i>faulty transformers</i> valued at about KSh 4.6 bilion.	Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma (DPP) anasema jumla ya mameneja kumi na mmoja wa kampuni hiyo wanakabiliwa na tuhuma za kutekeleza uhalifu wa kiuchumi. Mameneja hao wanatuhumiwa kushirikiana kununua <i>vifaa ovyo</i> vya KSh 4.6 bilioni na kusababisha kupotea kwa pesa za umma.	<i>tuko.com</i>
President Emmerson Mnangagwa's party is poised to win a substantial parliamentary majority in Monday's poll-the first elections since long-serving rule Robert Mugabe was ousted ... Common Market for Eastern and Southern Africa (Comesa) praised the electoral commission for using <i>biometric kits</i> to register voters, saying it reduced the possibility of multiple voting.	Chama cha rais Emmerson Mnangagwa kinaelekea kupata ushindi mkubwa wa viti vya bunge katika uchaguzi mkuu wa Jumatatu -ukiwa ni uchaguzi mkuu wa kwanza tangu aliyekuwa kiongozi wa muda mrefu Robert Mugabe kuondoka madarakani ... Muungano wa Comesa ulisifu tume ya uchaguzi kwa kutumia <i>kifaa cha Biometric</i> kusajili wapiga kura akisema kuwa kimepunguza uwezekano wa watu kupiga kura zaidi ya mara moja.	<i>bbc.com</i>

Katika matini ya kiuchumi iliyonukuliwa kwenye jedwali hili, matini *faulty transformers* imetafsiriwa sawa na *vifaa ovyo*. Kwa kukosa kupata kisawe cha neno *transformer*, mfasiri ameamua kutumia *vifaa* ambalo ni neno

linalotoa dhana ya kijumla sana. *Vifaa* hurejelea zana nyingi za kufanya kazi tofautitofauti katika sekta mbalimbali huku *transformer* ikiwa mtambo mahsusi wa kusambaza umeme. Baada ya kukosa kisawe mwafaka, mfasiri angetohoa istilahi *transfoma ghushi* ili kudumisha maana wasilifu. Msamiati mwingine wa sayansi na teknolojia ambao mfasiri amekwepa kutafsiri ni *biometric kits*. Katika kuhawilisha istilahi hii, mfasiri amehulutisha LC na LL na kuihawilisha kama *kifaa cha Biometric* katika ML. Mkakati wa kutumia ufafanuzi kufidia maana kwa kurejelea istilahi hii kama *mtambo wa kutambua wapiga kura ungeifaa HL*.

Ugumu wa kupata visawe vinavyohodhi dhana zinazotokana na LC huweza kumlazimisha mfasiri kukwepa kutafsiri neno husika, hivyo, kulidondosha anapozalisha ML. Hali hii inaweza kupoteza maana inayowasilishiwa HL. Tazama istilahi ya kiutabibu iliyodondolewa kutoka *tuko.com* katika Jedwali Na. 3 lifuatalo:

Jedwali Na. 3: Udondoshaji wa Istilahi ya Kisayansi

Matini Chanzi	Matini Lengwa	Chanzo
<p>Troubled Pumwani <i>Maternity</i> Hospital has received a life line after Nairobi Governor Mike Sonko signed a deal with Aga Khan and Nairobi West hospitals to transform the facility. The county boss held a meeting with the top management of Aga Khan University Hospital on Friday, September 21, where they agreed to provide additional doctors, nurses and support staff for a period of two years at no cost.</p>	<p>Ni habari njema kwa wagonjwa wa Pumwani baada ya gavana wa Nairobi Mike Sonko kutia sahihi mkataba na Hospitali ya Aga Khan na Nairobi West, kubadilisha hospitali hiyo. Msimamizi huyo wa kaunti alifanya mkutano na usimamizi wa Aga Khan University Ijumaa, Septemba 21, ambapo walikubaliana madaktari zaidi, wauguzi na wahudumu kwa muda wa miaka miwili watatolewa na Aga Khan.</p>	<p><i>tuko.com</i></p>

Kulingana na matini hii, istilahi *maternity* imedondoshwa katika ML. Ujumbe unaodhihirika katika matini hii ni kuwa Hospitali ya Pumwani ni taasisi inayotoa huduma mahsusi za matibabu. Kusema hivi ni kumaanisha kuwa hospitali hii imejengwa kwa madhumuni ya kuwahudumia wanawake wajawazito kwa kuwatibu na kuwazalisha. Hii ina maana kuwa taasisi hii haina uwezo wa kuwahudumia wagonjwa wowote wale walio na matatizo mengineyo ya kiafya. Ni wazi kwamba unyofojaji wa neno hili katika ML umeipunja HL taarifa muhimu. Taaluma ya utabibu ina msingi wake katika sayansi yenye chimbuko lake katika nchi zilizoendelea. Kwa hiyo, ina ubaidifu na Kiswahili.

Waaidha, muktadha wa dondoo la matini hii una aya nzima inayohusu vifaa na huduma za matibabu ambayo hajatafsiriwa kutokana na kauli kuwa vifaa na huduma hizi zinarejelea taaluma ya utabibu wa kisayansi ambao hauna uyaakinifu na LL. Tazama Jedwali Na. 4 lifuatalo.

Jedwali Na. 4: Udondoshaji wa Matini ya Kiutabibu katika ML

Matini Chanzi	Matini Lengwa	Chanzo
<p>“The proposed Sonko health facility shall cover a total area of 39,699 m² and a 450 beds capacity that will offer the following levels of care: Surgeries procedures, deliveries, immunization, inpatient beds with 24 hrs emergency services and high end diagnosis services,” he added. The labour wards shall contain delivery suites with four functional ward theatres, a post-natal ward, a newborn unit with 100 incubators including neonatal ICU, 20 Neonatal HDU with 30 procedure rooms for breastfeeding. The radical changes and proposals came amid ongoing investigations into the circumstances surrounding the death of 11 newborn babies which were discovered by the governor after he stormed the hospital.</p>	-	<i>tuko.com</i>

Mfasiri amepata ugumu kutafsiri istilahi kama vile *Surgeries, procedures, deliveries, high end diagnosis services, labour wards, delivery suites, ward theatres, post-natal ward, newborn units, incubators, neonatal ICU, Neonatal HDU* na *procedure rooms*, na, hivyo, kulazimika kuzidondosha katika ML. Yawezekana mfasiri alikwepa kufasiri sehemu hii ya matini kutokana na umilisi mfinyu wa LC na istilahi za taaluma ya utabibu. Kutokana na udondoshaji huu wa matini za utabibu, maarifa yanayohusu

vifaa na huduma muhimu za afya hazijafikia HL kutokana na maana kupotea. *“Hospitali ya Sonko iliyopendekezwa itajengwa katika ardhi yenye ukubwa wa 39,699 m² na itatoa huduma zifuatazo: Upasuaji, kujifungua, chanjo, huduma kwa wagonjwa wa kulazwa na huduma za dharura kwa saa 24, na huduma za hali ya juu za upimaji wa maradhi,”* alisema. Wadi za wanawake wajawazito zitakuwa na vyumba vya kujifungulia, wadi ya wanawake waliojifungua, sehemu ya watoto waliozaliwa iliyo na mitambo 100 ya kukuza watoto pamoja na Wadi ya Watoto walio Mahututi, Wadi 20 za Watoto Mahututi Wanaohitaji Uangalizi Maalum yenye vyumba 30 vya kunyonyeshea watoto. Mapendekezo ya mabadiliko hayo makuu yalitokana na uchunguzi unaoendelea kuhusu vifo vya wakembe 11 waliogunduliwa na gavana alipoitembelea hospitali hiyo” ni tafsiri ambayo ingeifaidisha HL.

Mfasiri anaposhindwa kabisa kuelewa dhana inayokusudiwa na neno fulani, anaweza kufungia nje neno hilo hasa pale ambapo udondoshaji huo hauathiri pakubwa maana ya matini kwa jumla. Klyukanov (1995) anataja udondoshaji wa vipashio vya lugha kama mkakati unaoweza kutumiwa ili kuyakinisha ujumbe katika tafsiri. Hata hivyo, hatua ya mfasiri kufutilia mbali neno anaposhindwa kung’amua maana yake haichukuliwi kama mkakati wa kukabiliana na changamoto ya tafsiri ila anapofanya uamuzi huo kimakusudi (Kimutai, 2016). Mtaalamu huyu anasema zaidi kuwa maneno yanayozua haja ya kudondoshwa ni kama maneno mwambatano, istilahi za taaluma mahsus ambazo ni ngumu kutafsiri, na maneno yanayokwenda kinyume na miiko ya LL kwa kukorofisha mbeko za jamii ya LL. Musau (2000) naye anadokeza kuwa lugha nyingi ikiwemo Kiswahili zina upungufu wa maneno au istilahi zinazohitajika kufanikisha

mawasiliano katika nyanja na taaluma za kisasa kama vile sayansi, sheria, biashara, na spoti miongoni mwa nyingine.

Uchanganuzi huu umebainisha kuwa ukosefu wa visawe vya kisayansi na kiufundi katika LL huzua changamoto kubwa katika kadhia ya tafsiri. Hali hii imesababisha matini nyingi kudondoshwa katika ML. Pale ambapo zimetafsiriwa, pametokea upotofu wa maana kufuatia uteuzi wa visawe visivyoweza kuakisi dhana husika. Matokeo yake ni kwamba ama HL imepunjwa ujumbe kamili pale ambapo misamiati hii imedondoshwa au maana kupotoshwa pale ambapo pametokea uteuzi wa visawe visivyowasilisha ujumbe kwa utoshelevu.

Tafsiri tenge ya msamiati ibuka

Mojawapo ya sifa bia za lugha ni ukuaji wake. Kukua kwa lugha kunasababishwa na kuibuka kwa dhana mpya katika ulimwengu wa mwanadamu kutokana na maendeleo ya kiteknolojia, kiuchumi, kisiasa na kijamii (Iribemwangi na Mukhwana, 2011). Mbali na ubunaji, msamiati mpya huweza kuzuka kufuatia hali ya maneno yaliyozoeleka kutanuliwa na kupewa matumizi mapya ya kimuktadha. Akichunguza utoshelevu wa mawasiliano kwa Kiswahili katika teknolojia ya SIKANU, Stephano (2020) amegundua uundaji wa msamiati mpya wenye dhima ya kuziba mwanya wa mawasiliano unaotokana na uvumbuzi wa mambo mapya. Anasema zaidi kuwa haja ya kukidhi mawasiliano imesababisha baadhi ya vitenzi vilivyotumiwa katika mawasiliano ya *WhatsApp* kupewa maana mpya. Kwa upande wao, Ipara na Maina (2008) wanasema kuwa, wakati mwingine, katika upekee wake, lugha hukosa kukidhi mahitaji ya watumiaji wake katika nyanja zote za mawasiliano. Kwa hiyo, wakati mwingine, lugha

huhitaji au hulazimika kujiumbua ili kutimiza mahitaji haya mapya yanayoendelea kuchipuka nje ya mawanda ya kawaida (Musau, 2000).

Kwa upande wake, Massamba (1987) anaeleza kuwa uibuaji wa maana ya maneno na kauli isiyozeleka huweza kutokana na mazoea ya matumizi yake kwa njia fulani na pia maendeleo au mabadiliko yanayotokea katika nyanja mbalimbali za maisha. Kwa sababu ubunaji wa msamiati mpya wa kurejelea dhana ngeni ni mchakato unaochukua muda, mfasiri hujikuta kama hana maneno ya kurejelea dhana hizo, na, hivyo kulazimika kutumia tafsiri ya neno kwa neno kuzitafsiri. Hata hivyo, tafsiri ya aina hii, aghalabu, hukengeusha maana ya dhana hizo. Mfano ufuatao wa matini iliyonukuliwa kutoka jukwaa la *tuko.com* unaonesha tafsiri ya misamiati ibuka katika sajili ya siasa nchini Kenya.

Jedwali Na. 5: Tafsiri ya Misamiati Ibuka katika Matini ya Siasa

Matini Chanzi	Matini Lengwa	Chanzo
<p>Ruto feeling Raila’s presence in Jubilee 3 months after dismissing him...Ruto has, however, sounded the alarm claiming that Raila is plotting a scheme to oust him from the party. The ODM camp, however, blamed Ruto for Planning to sabotage <i>Building Bridges Initiative</i> ... This emerged during the wake of the March 2018 <i>handshake</i> between Raila and President Uhuru Kenyatta ... Sentiments made by the DP on Sunday, September 30, as he addressed citizens at the coastal region, however, strongly suggested Ruto seems to be shaken by the <i>handshake</i>.</p>	<p>Ruto ameanza kuhisi uwepo wa Raila ndani ya Jubilee miezi 3 baada ya kudai kuwa hamtambui ... Hata hivyo, Ruto amelalama kuwa Raila alijiunga na Jubilee kwa lengo la kutaka kusambaratisha chama hicho na kuhakikisha kwamba amefurushwa. Aidha, wabunge wa ODM wamemshutumu Ruto kwa kutaka kuhujumu <i>mradi maalum wa Bridging the gap</i> ambao ulizinduliwa na Rais Uhuru Kenyatta ... Haya yalijiri baada ya Raila na Rais Uhuru Kenyatta <i>kusalimiana</i> mwezi Machi na kuamua kufanya kazi kwa pamoja ... Inaonekana Ruto amejawa na wasiwasi tangu Raila <i>alipoamua kufanya kazi na Jubilee</i>.</p>	<p><i>tuko.com</i></p>

Katika MC, kuna matumizi ya neno *handshake*. Neno hili limetafsiriwa moja kwa moja kama *kusalimiana* na vilevile kama *alipoamua kufanya kazi na Jubilee*. Tafsiri hizi tofauti zimekengeusha maana katika ML. Msamiati *handshake* ulizuka mwezi Machi mwaka 2018 katika medani za kisiasa nchini Kenya baada ya wapinzani wakuu katika uchaguzi mkuu uliokumbwa na utata wa mwaka 2017, Rais Uhuru Kenyatta na Raila Odinga kukutana na kufanya mashauriano ya kuridhiana kutokana na uhasama ulioletwa na matokeo ya uchaguzi huo. Viongozi hawa wawili

hawakusalimiana tu, walifikia mwafaka wa kisiasa ambao umewaunganisha na kuwapatanisha. Maridhiano hayo yalidhamiriwa kuwawezesha viongozi hao wawili kusameheana, kufanya kazi pamoja, na kuunganisha nchi iliyokwishagawanyika kutokana na uhasama wa kikabila ulioletwa na misimamo tofauti ya kisiasa. Ni kwa msingi huu ambapo tafsiri nyingine ya *handshake* kama *alipoamua kufanya kazi na Jubilee* katika ML, kwa kiasi fulani, inaelekea kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa.

Ili kuepuka upotoshaji wa maana ya misamiati ibuka, wafasiri wengine huamua kuchakata misamiati hii kwa kuitolea maelezo yanayotagusanisha LC na LL au kwa kuitumia jinsi ilivyo katika MC. Kutokana na ugeni wa msamiati *Building Bridges Initiative*, mfasiri ameamua kuutafsiri sawa na *mradi maalum wa Bridging the gap* ili kudumisha maana yake. Msamiati huu nao ulizuka mnano Machi 2018 pale ambapo, kufuatia maridhiano ya kisiasa, Rais Uhuru Kenyatta na mpinzani wake Raila Odinga waliunda jopo la wataalamu lenye jukumu la kutafuta maoni ya wananchi kuhusu mabadiliko ya kikatiba yanayohitaji kufanyika katika uongozi wa nchi ili kufikia maendeleo na mshikamano wa taifa.

Kulingana na matini hii, Naibu wa Rais, William Ruto, anakashifiwa na wabunge wa chama cha *Orange Democratic Party (ODM)* kwa kuhujumu shughuli za jopo hili kwa kuhofia kuwa kufanikiwa kwake kunaweza kubadilisha nafasi za uongozi nchini na kumzuia kuwa rais wa Kenya au kupunguza ushawishi wake baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2022. Kwa hiyo, ‘Aidha, wabunge wa *ODM* wamemshutumu Ruto kwa kutaka kuhujumu *harakati za mapatano* ambazo zilizinduliwa na Rais Uhuru Kenyatta. ... Haya yalijiri baada ya Raila na Rais Uhuru Kenyatta *kuridhiana* mwezi Machi na kuamua kufanya kazi kwa pamoja...

Inaonekana Ruto amejawa na wasiwasi tangu Raila *alipoamua kushirikiana na Jubilee*’ ni tafsiri ambayo ingeyakinisha maana kwa ufanisi zaidi.

Katika harakati za kudumisha dhana zilizokusudiwa katika MC, wakati mwingine, wafasiri huzalisha ML bila kutafsiri msamiati ibuka. Hata hivyo, uhamishaji huu wa maneno ya LC katika ML huweza kutatiza HL isiyo na umilisi mpevu wa LC. Haya yamebainika katika matini ifuatayo ya kijamii kuhusu mapenzi kutoka jukwaa la *tuko.com*.

Jedwali Na. 6: Tafsiri ya Misamiati Ibuka katika Matini ya Kijamii

Matini Chanzi	Matini Lengwa	Chanzo
The murder of Rongo University student is a lesson to girls, leave <i>sponsors</i> alone-MP Gladys Wanganga...Homa Bay Women Representative Gladys Wanganga has strongly condemned the murder of Rongo University student, Sharon Otieno, and warned ladies to keep off old men and focus on their lives...Speaking to journalists at Parliament buildings on Wednesday, August 5, the MP asked young women to accept their humble backgrounds and focus on working hard to improve their lives instead of relying on <i>sponsors</i> .	Someni achaneni na maisha ya ' <i>sponsor</i> ' mtaangamia-Gladys Wanganga... Mwakilishi wa kike wa Homa Bay Gladys Wanganga amekashifu mauaji ya mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Rongo, Sharon Otieno, na kuwaonya wasichana dhidi ya kuwafuatafuata wanaume wa umri mkubwa...Akizungumza na wanahabari katika majengo ya Bunge Jumatano, Septemba 5, mbunge huyo alisema ni bora kwa wasichana kutia bidii masomoni badala ya kufuatana na wanaume wazee eti ' <i>sponsors</i> .'	<i>tuko.com</i>

Katika MC, pametumika neno *sponsors*. Huu ni msamiati uliozuka nchini Kenya na kutumika katika sajili ya mapenzi kuanzia mwaka wa 2018. Neno hili limehamishwa katika ML bila kutafsiriwa. Mfasiri amekwepa kulitafsiri kwa kukosa kisawe mwafaka ambacho kingehifadhi dhana inayowasilishwa nalo. Neno hili linatumika kwa maana ya wazee wenye ukwasi wa kifedha ambao huwanyemelea wasichana wachanga kwa kutumia pesa zao kama chambo. Kulingana na matini hii, Mwakilishi wa Kike wa kaunti ya Homa Bay, Bi. Gladys Wanganga, anawaonya wasichana dhidi ya kuhusiana

kimapenzi na wanaume wa umri mkubwa na badala yake kuwashauri kumakinikia masomo yao ili kufaulu maishani.

Kwa sababu ya ugeni wa dhana hizi, jumbe zinazopitishwa kutokana na matumizi yake zinaeleweka vema katika LC. Kinachomaanishwa hapa ni kuwa istilahi hizi zimetumika katika asili yake ili kuhakikisha kuwa hakuna upotofu wa jumbe zinazowasilishwa na misamiati hii ibuka. Hata hivyo, ujumbe unaowasilishwa katika ML huweza kukanganya HL isiyo na umilisi mpevu wa LC.

Ugumu wa kutafsiri misamiati ya TEHAMA

TEHAMA ni uwanja mwingine ambao umeshuhudia mfumko wa misamiati katika miaka ya hivi karibuni. Ugumu wa kupata visawe halisi vya maneno yanayotokana na maendeleo katika uwanja huu umepelekea ukopaji wa misamiati husika katika LL ili kuepuka kukengeusha maana zake. Hali hii inajitokeza katika Jedwali Na. 7 lifuatalo.

Jedwali Na. 7: Ukopaji wa Misamiati ya TEHAMA

Matini Chanzi	Matini Lengwa	Chanzo
<p>“It’s always a great pleasure meeting with one of Kenya’s most famous sons, President Barack Obama. He spoke very passionately about his foundation and particularly the empowerment of the youth and I commend both him and his sister Auma Obama for the commendable job,” Raila said in <i>a facebook post</i> seen by TUKO.co.ke on Sunday.</p>	<p>“Kila mara ni furaha kubwa mno kukutana na mtoto wa Kenya ambaye ni maarufu sana, Rais Barack Obama. Alizungumza kwa makini sana kuhusu msingi na hasa kuwawezesha vijana na nawashukuru sana wote, yeye na Auma Obama kwa kazi nzuri wanayofanya,” Raila alisema kupitia <i>ujumbe wa Facebook</i> ambao TUKO.co.ke iliisoma Jumapili.</p>	<i>tuko.com</i>
<p>Mourinho has attempted to underline his authority after an error by Pogba led to Wolves’ equaliser at Old Trafford on Saturday and the player’s subsequent comments criticizing United’s tactics. Pogba tried to play down his comments in <i>tweet</i> on Monday.</p>	<p>Mourinho amejaribu kuonyesha uzito wake baada ya kosa la Pogba kuisaidia timu ya Wolves kufunga bao la kusawazisha katika uwanja wa Old Trafford siku ya Jumamosi mbali na mchezaji huyo kukosoa mbinu zinazotumika. Pogba alijaribu kupuuzilia mbali matamshi yake katika <i>mtandao wa twitter</i> siku ya Jumatatu.</p>	<i>bbc.com</i>

Istilahi zinazotokana na maendeleo ya kiTEHAMA na kutumiwa katika matini kwenye Jedwali Na. 7 ni *Facebook* na *Twitter*. Katika matini hizi, *a facebook post* na *tweet* zimetafsiriwa sawa na *ujumbe wa Facebook* na *mtandao wa twitter*, mtawalia. Istilahi hizi za kiTEHAMA zimetafsiriwa

kwa kuchanganya lugha ya Kiingereza na Kiswahili kwa sababu hazina visawe rasmi katika LL. Kwa mujibu wa Muysken (2000), uchanganyaji msimbo huwa na dhima katika usemi. Ametambua dhima ya kurejelea, kufafanua, kupendeza na kujitambulisha, kuonyesha hisia, na kusisitiza. Matumizi katika matini hizi yamebainisha dhima ya kurejelea dhana ngeni ili kudumisha uasilia wake wa kisemantiki unaohakikisha uhifadhi wa ujumbe.

Kwa upande mwingine katika uzalishaji wa ML, badala ya kutumia istilahi za kiTEHAMA katika LC kutokana na ugumu wa kupata visawe vyake, wafasiri, wakati mwingine, huamua kudondosha istilahi hizi katika ML ili kuepuka utata unaoweza kutokana na ufasiri wa maneno ya lugha ngeni. Tazama matini ifuatayo ya kijamii kutoka jukwaa la *tuko.com*.

Jedwali Na. 8: Udondoshaji wa Msamiati wa Tehama

Matini Chanzi	Matini Lengwa
<p>Controversial socialite Huddah Monroe took to social media on Thursday 5, to boast about how only ‘big things’ makes her heart skip a beat ... In an <i>Instagram post</i> seen by Tuko.co.ke, the pretty young thing revealed she can only roll the sheets with men who have a huge package.</p>	<p>Sosholaiti tajika Huddah Monroe alijimwaya mtandaoni Alhamisi kusifia jinsi anavyowapenda wanaume wenye viazi vinono ... Katika <i>chapisho</i> lake lilioonwa na jarida la TUKO.co.ke, Huddah alieleza kuwa yeye huweza kuchovyana asali na wanaume wenye viazi vinono pekee.</p>

Kwa mujibu wa matini katika Jedwali Na. 8, *Instagram post* imerejelewa kama *chapisho*. Kwa hiyo, mfasiri amekwepa kutafsiri neno ‘Instagram’ huku akitafsiri neno ‘post.’ Kudondoshwa kwa istilahi hii kumbana wenzu uliotumiwa na Huddah Monroe kupitisha ujumbe kwa wasomaji. Kimutai

(2016) anasema kuwa mfasiri anaposhindwa kabisa kuelewa dhana inayokusudiwa na neno fulani, anaweza kufungia nje neno hilo hasa pale ambapo udondoshaji huo hauathiri pakubwa maana ya matini kwa jumla. Sangili na Obuchi (2019) nao wanasema kuwa maneno yanaweza kudondoshwa katika matini yanapokosa thamani ya ujumbe. Hata hivyo, katika muktadha huu, hatua ya kudondosha istilahi hii ya kiTEHAMA imeathiri maana kwa kuipunja HL taarifa inayohusu wenzu uliotumiwa na sosholaiti huyu kuwasiliana na mashabiki wake.

Hitimisho

MK yamekuwa wenzu muhimu wa kutandawazisha taarifa mbalimbali kupitia tafsiri katika kizazi cha kisasaleo. Hata hivyo, imebainika kuwa tafsiri ya matini nyingi zinazowasilishwa katika majukwaa haya imekumbwa na changamoto, na, hivyo kuwa kengeushi. Ukakasi wa kitafsiri ulioishia kutatiza maana ulitokana na tofauti za kiutamaduni kati ya LC na LL, uchechefe wa visawe vya kisayansi na kiufundi, tafsiri tenge ya misamiati ibuka na ugumu wa kutafsiri misamiati ya kiTEHAMA. Kwa hiyo, pana haja ya kuweka mikakati ya kuboresha tafsiri ya matini tepe zinazotafsiriwa katika MK ili kuhakikisha usadifu wa jumbe zinazowasilishwa kwa HL katika harakati za kufanikisha mawasiliano timilifu.

Marejeleo

Cartford, J. (1965). *Linguistic Theory of Translation*. London: Oxford University Press.

Elyildirim, S. (2008). The Importance of Cultural Knowledge in Translation: A Partial Replication of Olk 2003. *Sosyal Bilimler Dergisi*, 1, 131 - 144.

- House, J. (2016). *Translation as Communication across Languages and Cultures*. New York: Routledge Taylor & Francis Group.
- Ipara, I.O. & Maina, G. (2008). *Fani ya Isimujamii kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Oxford University Press.
- Iribemwangi, P.I. & Mukhwana, A. (2011). *Isimujamii*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.
- Jilala, H. (2016). Uhakiki wa Nadharia ya *Skopos* katika Tafsiri: Mifano ya Tafsiri ya Matini za Kiutamaduni. Katika H. Jilala. (Mh.). *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istihahi* (Kur. 70 - 91) Dar es Salaam: Daud Publishing Company Ltd.
- Kihore, Y.M. (2005). Uzingatifu wa Sarufi katika Tafsiri. *Swahili Forum*, 12, 109 - 120.
- Kimutai, K.H. (2016). Ulinganifu wa Taarifa za Habari: Tathmini ya Tafsiri kutoka Kiswahili hadi Kipsigis katika Kituo cha Kitwek, (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu Cha Nairobi.
- Klyukanov, I. (1995). Pragmatic Adaptation and the Translation of Culture. *Studies in Humanities*, 22(1 and 2), 21 - 32.
- Larson, M.L. (1984). *Meaning Based Translation: A Guide to Cross-language Equivalence*. New York: University Press of America.
- Massamba, D.P.B. (1987). The Impact of Politics in Language Development in Tanzania. *Kiswahili* 54,180 -191
- Matundura, B.E. (2007). Taaluma ya Tafsiri katika Vyombo vya Habari Nchini Kenya: Matatizo, Changamoto na Mustakabali Wake. Katika Njogu, K. (Mh.). *Kiswahili na Elimu Nchini Kenya*. Nairobi: Twaweza Communications. Kur 158 -168.
- Munday, J. (2001). *Introducing Translation Studies: Theories and Application*. London: Routledge.

- Musau, P. (2000). The Development of Swahili Styles: The Use of Metaphor in the Language of Football Commentary. Katika K. Njogu, C. Momanyi, K. King'ei & P. Musau. (Wah.). *Kiswahili katika Karne ya Ishirini na Moja*. Nairobi: Twaweza Communications Ltd. pp. 243 - 250.
- Musyoka, E.N. (2019). *Non-equivalence in the Kikamba Bible Translation*. PhD Thesis, Chuka University (Unpublished).
- Muysken, P. (2000). *Bilingual Speech: A Typology of Code-switching*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Mwansoko, H.J.M. (2016). Ukuzaji wa Kiswahili kupitia Tafsiri: Hatua Moja Mbele, Mbili Nyuma. Katika Jilala, H. (Mh.) *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istihahi*. (Kur 2 -18) Dar es Salaam: Daud Publishing Company Ltd.
- Mwansoko, H.J.M., Mekacha, R.D.K., Masoko, D.L.W., & Mtesigwa, P.C.K. (2006). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu* (Toleo la Pili). Dar es Salaam: TUKI.
- Newmark, P. (1988a). *Approaches to Translation*. London: Prentice Hall.
- Newmark, P. (1988b). *A Textbook of Translation*. Claredon: Multilingual Matters.
- Newmark, P. (1991). *About Translation*. Clevedon/Toronto: Multilingual Matters Ltd.
- Nida, E.A. & Taber, C.R. (1982). *The Theory and Practice of Translation* (2nd ed.). Leiden: E. J. Brill.
- Nida, E.A. (1964). *Towards a Science of Translating*. Leiden: E. J. Brill.
- Oduori, W.R. (2008). Uchunguzi wa Nadharia za Tafsiri: Mwelekeo wa Kiusemezano. Katika Ogechi, N.O., Shitemi, N.L. na Simala, K.I. (Wah.). *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika* (Kur. 333 - 34) Eldoret: Moi University Press.

- Safko, L. & Brake, D. (2009). *The Social Media Bible: Tactics, Tools and Strategies for Business Success*. New Jersey: John Wiley and Sons.
- Sangili, N.K.N. & Obuchi, S.M. (2019). Uhakiki wa Tafsiri ya Istitlahi za Kiufundi. Katika J. Kobia., M. Kandagor., L.C. Mwita., J.N. Maitaria & P.S. Wandera-Simwa. (Wah.). *Uwezeshwaji wa Kiswahili kama Wenzu wa Maarifa* (Kur. 39 - 48) Eldoret: Moi University Press.
- Shitemi, N. L. (2007). Taswira za Tafsiri, Mielekeo ya Ufundishaji na Maendeleo katika Taaluma ya Kiswahili. Katika Njogu, K. (Mh.) *Kiswahili na Elimu Nchini Kenya* (Kur 135 -157) Nairobi: Twaweza Communications.
- Shiyab, S. (2006). *A Textbook of Translation: Theoretical and Practical Implications*. Antwerpen: Garant Publishers.
- Stephano, R. (2020). Utochelevu wa Mawasiliano kwa Kiswahili katika Teknolojia ya SIKANU: Uchunguzi Kifani wa *WhatsApp*. *JULACE*, 5(1), 1 - 14.
- Tam, J. W., Tang, W. S. & Fernando, D. J. S. (2007). The Internet and Suicide: A double edged tool. *In European Journal of Internal Medicine*, 18: 453 - 455. New York: Oxford University Press.
- TUKI (2006). *English-Swahili Dictionary*. Dar-es-Salaam: TUKI.
- TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Toleo la Tatu. Dar-es-Salaam: Oxford University Press, East Africa Ltd.
- Wanjala, F.S. (2011). *Misingi ya Ukalimani na Tafsiri kwa Shule, Vyuo na Ndaki*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.
- Waters, J.K. & Lester, J. (2010). *The Everything Guide to Social Media: All You Need to Know about Participating in Today's Most Popular Online Communities*. Avon, MA: Adam Media.